TANGAZO LA HABARI
KIKWAZO Juni 18 10:30am CET

# Mawasiliano ya Simu ya Rununu ili Kupindua Ufuatiliaji wa Hali ya Hewa ya Afrika

- Baraza la Wahisani Ulimwenguni, Ericsson, WMO, na Zain na opereta wengine wa simu za rununu kuweka hadi vituo atomati 5,000 vya hali ya hewa katika maeneo ya mtandao rununu Afrika kote, ambapo chini ya vituo 300 vimeripotiwa hadi wa sasa

- Ubia utaongeza usambazaji wa maelezo ya hali ya hewa kupitia simu za rununu kwa watumiaji na jamii, pamoja na wakulima na wavuvi wa mashambani

- Vituo 19 vya kwanza viliwekwa zaidi ya mara mbili ili kufuatilia hali ya hewa ya eneo la Ziwa Viktoria, ambapo watu 5,000 hufa kila mwaka kutokana na dhoruba na ajali

GENEVA, Juni 18, 2009 – Baraza la Wahisani Ulimwenguni na Rais wake, Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa Kofi Annan, pamoja na Ericsson, Shirika la Metolojia Ulimwenguni ( WMO), kampuni ya mawasiliano ya simu za rununu ya Zain, na Taasisi ya Ardhi katika Chuo Kikuu cha Columbia, walitangaza leo uvumbuzi mkubwa, uliopewa jina la "Maelezo ya hali ya hewa kwa wote", ili kuboresha pinduani mtandao wa kufuatilia hali ya hewa ya Afrika katika wajihi wa ukuaji mkubwa wa athari ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Ripoti ya hivi karibuni ya Baraza la Wahisani Ulimwenguni ilikadiria kwamba kubadilika kwa hali ya hewa kunawajibika kwa vifo 300,000 kila mwaka na hasara za kiuchumi za thamani ya zaidi ya dola bilioni 100 za Marekani, haswa kwa sababu ya mishtuko ya kiafya na uzalishaji wa ukulima. Sahara Kusini mwa Afrika inahusishwa na karibu robo ya hasara hizi, na ndio eneo lenye hatari ya sasa ya ukame na mafuriko. Mazao ya ukulima katika maeneo mengine yanatarajiwa kupungua kwa asilimia 50 mapema mwaka wa 2020.

Baraza la Wahisani Ulimwenguni lilianzisha ushirikiano huu ili kujibu pengo kubwa la Afrika la maelezo ya hali ya hewa lililoangaziwa katika hafla ya kwanza ya baraza kila mwaka. Washirika wa uvumbuzi huo wataweka hadi vituo otomati 5,000 mpya vya kufuatilia hali ya hewa kote Afrika, vitakavyosaidia kutoa ongezeko kubwa katika habari muhimu za kutabiri na kusimamia mishtuko ya hali ya hewa.

Afrika ina mfumo wa mtandao mara nane chini ya kiwango cha chini zaidi kinachopendekezwa na WNO, na chini ya vituo 200 vya hali ya hewa ambavyo vinafikia mahitaji ya ufuatiliaji ya WMO, ikilinganishwa na maelfu kadhaa katika Uropa, Marekani, Kaskazini, na sehemu za Asia. Vituo hivyo 5,000 vitasanidiwa kwenye maeneo mapya na yaliyomo ya mtandao wa simu za rununu barani kote kati ya miaka ijayo, kwa ile inayoahidi kuokoa maisha na kuleta ongezeko la nafasi za kiuchumi kwa kumi ya mamilioni ya watu.

Ubia binafsi -umma wa uvumbuzi kwa uzani wa kipekee, uvumbuzi unategemea biashara kuu ya mawasiliano. Ericsson, mtoaji anayeongoza wa vifaa na huduma za mawasiliano ulimwenguni, itahusiana na opereta wa Afrika kama Zain ambao watafadhili vifaa vya hali ya hewa katika maeneo ya mtandao wa simu za rununu yanayotolewa Afrika kote. Kufikia lengo la 5,000 kunahitaji kujitolea zaidi kwa opereta na ufadhili wa nje.

Uzinduzi ulifanyika katika Jukwaa la Ulimwengu la Upunguzaji Hatari ya Maafa, ambapo Kofi Annan alisema:

> " Walio maskini zaidi ulimwengu ndio pia wanaweza kuathiriwa zaidi wakati wa athari za mabadiliko ya hali ya hewa, na ambao hawana vifaa vyovyote vya kukabiliana na matokeo yake. Leo utapata minara ya simu za rununu karibu kwa kila eneo la Afrika. Hatujawahi kuweza kuanzisha ufuatiliaji wa hali ya hewa katika kiwango hicho, hadi sasa. Kwa kuleta pamoja wataalam na rasilimali za wachezaji tofauti wa umma na binafsi, mradi huu unaweza kusaidia kuokoa maisha na kuboresha hali ya maisha ya jamii za Afrika zilizo katika mstari wa mbele wa mabadiliko ya hali ya hewa.

Aliyekuwa pia katika uzinduzi, Rais na Afisa Mkuu Mtendaji wa Ericsson, Carl-Henric Svanberg, alisema:

> “ Ukuaji mkubwa wa watumiaji wa simu za rununu katika Afrika unaonesha nafasi bora zaidi kwa jamii ya mawasiliano ili kushirikiana na wabia wa kitaifa ili kuboresha mitandao ya hali ya hewa na mifumo barani kote.
>
> “ Kama mtoaji anayeongoza wa mawasiliano katika Afrika kwa zaidi ya miaka 100, tuko katika nafasi ya kipekee kudhibiti utoaji wa mitandao ya simu za rununu wakati tunaposaidia kupunguza athari ya kubadilika kwa hali ya hewa kwa walioathirika zaidi. Tunatarajia kuwa na opereta zaidi wanaojiunga ili kugundua athari kamili ya uzinduzi huo.”

Mitandao ya simu za rununu hutoa uunganisho unaofaa, umeme na usalama ili kuendeleza vifaa vya hali ya hewa. Kupitia Kituo chake cha Uvumbuzi wa Simu za Rununu katika Afrika, Ericsson pia itakuza programu tumizi za simu za rununu ili kusaidia kuwasilisha maelezo ya hali ya hewa inayokuzwa na huduma za metolojia na haidrolojia ( NMHS) kupitia simu za rununu. Opereta wa simu za rununu watatunza vituo atomati vya hali ya hewa katika usambazaji wa data kwa huduma za kitaifa za meteolojia.

Uwekaji wa kwanza tayari umeanza katika mitandao ya Zain, na inazingatia eneo karibu na Ziwa Viktoria nchini Kenya, Tanzania na Uganda. Vituo 19 vya kwanza vilivyosanidiwa vitaongeza mara mbili uwezo wa kufuatilia hali ya hewa ya eneo la Ziwa. Afisa Mkuu Mtendaji wa Zain Saad Al Barrak alisema:

> “ Kweli ni vizuri sana kwamba jamii nyingi Afrika kote sasa zitakuwa na habari sahihi zinazopatikana za meteolojia. Hapa tunaweza kuona jinsi jamii za simu za rununu zinaweza kuchukua jukumu kuu katika kusaidia kuboresha ubora wa maisha na usalama kwa watu katika maeneo ya mashambani ulimwenguni.”

Takriban asilimia 70 ya Waafrika wanategemea ukulima kwa maisha yao, au karibu watu milioni 700 na zaidi ya asilimia 95 ya wakulima wa Afrika wanategemea mvua. Kubadilika kwa mitindo ya hali ya hewa kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa hutoa maelezo ya kitamaduni yasiyotumika kuhusu ukulima ili kufaa kwa karne, ikiunda hitaji kubwa la maelezo ya meotolojia.

Aliyekuwa pia katika uzinduzi wa Geneva ni Katibu Mkuu wa WMO, Michel Jarraud, sauti ya utawala wa Mifumo ya Umoja wa Mataifa juu ya Hali ya Hewa, tabia ya nchi na Maji, ambayo inaratibisha kuhusika kwa NMHS inayohusika katika uvumbuzi. Bw. Jarraud alisema:

> “ Kwa uzalishaji wa chakula, karibu kila uamuzi unaunganishwa na vigezo vya hali ya hewa, tabia ya nchi na maji. Tunaona maelezo ya hali ya hewa kwa vumbuzi zote kama bidii kuu ya Afrika nzima ili kuwezesha Washirika wetu 188 kutoa habari na huduma ya hali ya hewa iliyoboreshwa. Kwa kufanya kazi kupitia NMHS, kwa hakika WMO itatambua mahitaji ya maelezo ya hali ya hewa, ushauri kuhusu mahitaji na itasaidia kusambaza habari hiyo. Uvumbuzi huu utathibitisha kuwa moja ya zile muhimu zaidi kwa meteolojia ya Afrika kwa miongo. Hivyo pia

> mradi utaunga mkono malengo ya Mkutano-3 uliopangwa na WMO- wa Hali ya hewa Ulimwenguni, utakayofanywa kuanzia tarehe 31 Agosti hadi tarehe 4 Septemba 2009 huko Geneva."

Uvumbuzi utakuwa na athari inayozidi matayarisho ya ukulima na maafa kwani ni pamoja na usaidizi wa huduma za kitaifa za meteolojia katika kufunza na uwezo wa kiufundi. Habari bora za hali ya hewa pia zitawezesha ukuzaji wa huduma, kama bima ndogo, ambayo inaweza kutegemea arafu za data ya hali ya hewa, kama mvua. Uvumbuzi huu pia utaongeza kiwango cha habari muhimu kwa wanasayansi, na hata pia tasnia ya maji, uchukuzi na nishati.

Kwa kuwa pengo la maelezo ya hali ya hewa ni mbaya sana katika Afrika, uvumbuzi utakuwa wazi kwa upanuzi wa baadaye katika maeneo yaliyoathirika.

Mbia zaidi katika uvumbuzi ni Taasisi ya Ardhi ya Chuo Kikuu cha Colombia, inayoongozwa na Jeffrey Sachs. Kusaidia na usambazaji wa sehemu kadhaa zilizoathirika na zilizo maskini zaidi katika Afrika na katika ubia na Taasisi ya Ardhi, vituo atomati vya hali ya hewa bado vitasanidiwa katika Vijiji vya Milenia – miradi ya mashambani ya ukuzaji itasambaaa kwa nchi 10 na kuzingatia kufikia Malengo ya Milenia ya Ukuzaji. Kwa kufikia wataalam Wanasayansi wa taasisi za Ardhi juu ya taaluma ya hali ya hewa, ukulima, na afya, mradi huo unatumaini kutambua maeneo msingi ambayo yanaweza kuathari kwa sasa na kuchangia hifadhi ya ufahamu kwa juhudi hiyo.

Jeffrey Sachs alisema:

> " Taasisi ya Ardhi ni mbia wa kujivunia katika mpango huu wa uvumbuzi wa hali ya juu," mkurugenzi wa taasisi Jeffrey Sachs, alisema, " Mara tu swichi inapowashwa, mtiririko mpana wa data za hali ya hewa utapatikana Afrika kote, na faida kutoka kwa watengenezaji sera za kitaifa kwa wakulima wadogo. Vijiji vya Milenia ni eneo bora la uzinduzi wa kweli na wa wakati mzuri wa data za hali ya hewa ili kuboresha unyumbukaji wa maendeleo endelevu katika Sahara kusini mwa Afrika."

MWISHO

MATINI KWA WAHARIRI:

Baraza la Wahisani Ulimwenguni na ripoti yake juu ya Ripoti ya Athari za Binadamu: Kubadilika kwa Hali ya hewa– Anatomy of Silent Crisis inapatikana kwenye: http://www.ghf-ge.org/programmes/human_impact_report/index.cfm, http://www.ghf-ge.org

Kwa maelezo yaidi kuhusu WMO na Mkutano wa 3 wa Hali ya hewa Ulimwenguni:

http://www.wmo.int, http://www.wmo.int/wcc3/index_en.html

Kwa maelezo yaidi kuhusu Zain, tafadhali tembelea www.zain.com au email info@zain.com

Soma zaidi kuhusu mradi wa vijiji vya milenia kwenye: http://www.millenniumvillages.org

KWA MAELEZO YAIDI, TAFADHALI WASILIANA NA

Baraza la Wahisani Ulimwenguni

| | |
|---|---|
| Simu | Keith Collins |
| | +41 22 919 75 48 |
| | +41 76 703 53 33 |
| | Annika Hartmann |
| | +41 22 919 75 17 |
| | Matthew McKinnon |
| | +41 79 500 35 08 |
| Barua pepe | media@ghf-ge.org |

**Ericsson**

Shirika la Umma na Mahusiano ya Vyombo vya Habari

| | |
|---|---|
| Simu | +46 10 719 69 92 |
| Barua pepe | press.relations@ericsson.com |

Zain

| | |
|---|---|
| Simu | Mwambu Wanendeya |
| | +973 3603 5799 |
| Barua pepe | Mwambu.wanendeya@zain.com |

Shirika la Meteolojia Ulimwenguni ( WMO)

| | |
|---|---|
| Simu | Carine Richard-Van Maele (Chifu, Maswala ya Mawasiliano na Umma) |
| | +41 (0) 22 730 83 15 |
| Barua pepe | cvanmaele@wmo.int |
| Faksi | + 41 (0) 22 730 80 27 |
| Simu | Gaëlle Sévenier |
| | +41 (0) 22 730 8417 |
| Barua pepe | gsevenier@wmo.int |
| Simu | Lisa Muñoz |
| | +41 (0) 22 730 82 |
| Barua pepe | lmunoz@wmo.int |

Taasisi ya Ardhi katika Chuko Kikuu cha Columbia

| | |
|---|---|
| Simu | Xkyu-Young Lee |
| | +1 646 337 3528 |
| Barua pepe | klee@ei.columbia.edu |